# K U T A K A S W A

*Waebrania 10:10: Katika mapenzi hayo tumepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

*Yohana Mtakatifu 17:17-19, "Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndio kweli. Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma ulimwenguni. Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli*"

Ni kitu gani? Oh Mungu anahitaji ukamilifu. Anahitaji toba yako. Anahitaji utiifu wako kwake. Lakini yeye anaangalia usiku wa leo. Haijalishi umetenda dhambi nyingi kiasi gani, ziwe kidogo au ziwe nyingi, wewe bado ni mdhambi, na huwezi ukaingia kwa njia yeyote ile isipokuwa kwa Yesu kristo. Sadaka itoshelezayo ya Mungu. Na ndani yake umekamilishwa milele. Fikiria hilo.

Siyo chochote kile unachofanya. Siyo kurasa mpya unazofungua, siyo maisha mapya unayoanza. Ni kule kuungama/kukiri makosa yako, na neema ya Mungu kwako. Hiyo inakuleta wewe kwenye ukamilifu, na tena unakamilishwa ndani ya Yesu Kristo.

Unasema "ndugu Branham, wakati nitakapoweza kuacha kuvuta nitakapo acha kulewa, nitakaponyoosha mambo haya nitafanya hivyo". Oh haitaweza kamwe kufanyika kwa usahihi. Hutaweza kamwe kulifanya hilo. Kwa nini usije tu jinsi hiyo ulivyo? Ni kwa Imani, uende kwenye kijito kile, kinacho tiririka kutoka vidonda vyake, halafu ni mafikirio yangu ya upendo unaookoa, na hayo yatakuwa mpaka utakapokufa.

Kwa nini uchukue kitu badala? Kwa nini uingie kupitia Kanisa lako? Kwa nini ujaribu kuja eti kwa sababu umeacha ulevi au umeacha uongo? Njoo kwa njia ya ukamilifu maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa. (Waebrania 10:14)

Nitawezaje kutakaswa? Ungama dhambi zako mbele ya Damu ya Yesu Kristo, na ule uhai utokao ndani ya Damu, unamrudia mwabudu na kumtakasa yeye kutoka kwenye tamaa za dunia. Maana kwa sadaka ile Kamili itoshayo ametutakasa sote, na kwa roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa mwili mmoja (1kor. 12:13). Kwa hiyo hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio ndani ya Yesu Kristo, ambao hawaenendi tena kwa kuufuata mwili bali Roho (Warumi 8:1). Kama unajaribu kutembea kwa Roho na bado unatamaa za mwili, ile sadaka haikupakwa kiasi cha kutosha kwako. Lakini mwabudu anapotakaswa hana shauku tena ya dhambi.

Hiyo ilikuwa ni Kalvari. Siyo sehemu ya kuuza mauwa au sehemu ndogo ya kufanya hivi au vile. Ilikuwa ni sehemu ambayo Mungu na mwanadamu walipatanishwa. Ilikuwa ni mahali ambapo Amani na usalama mkamilifu vililetwa kwa jamaa ya binadamu. Unaweza kwenda pamoja nami usiku huu wa leo, rafiki yangu mwenye dhambi, twende Kalvari/Msalabani, na kwa imani upake hii Damu katika nafsi yako mwenyewe, na umwache Roho Mtakatifu aje na akutakase wewe kwa sadaka yake kubwa? (2 Wathes. 2:13).

Kama kuna chochote ninachoweza kukifanya ili kujifanya mkamilifu mbele za Mungu, basi Kristo hakupaswa kufa kwa ajili yangu. Kama kuna chochote. Unachoweza kukifanya ambacho kingekustahilisha mbele za Mungu, basi Kristo alikufa bure. Hapana na kushika sheria, hakuna kanuni zozote za kwako za kisheria, siyo utakatifu wako mwenyewe. Hakuna vitu unavyoweza kuacha kuvifanya, kuacha uongo, kuacha kuiba, kuacha kuvuta tumbaku, kuacha kwenda kwenye sinema/video, bado umepotea. Hakuna kiwezacho kufanya hilo. Kujiunga na Kanisa, taratibu za ibada, sherehe, ubatizo, utaratibu wa Kanisa, kusoma Kanuni za imani, kusema maombi, mambo haya yote hayatahesabika kuwa ni kitu, wewe umepotea. Hakuna hata kitu kimoja uwezacho kufanya wewe mwenyewe, kwa sababu wewe ni mdhambi na upo chini ya hukumu. Na hakuna njia uliyonayo mwenyewe au kanuni yoyote au chochote ambacho unaweza kufanya, au kufikiri wewe mwenyewe, ambacho kingeweza kukustahilisha kimoja tu mbele za uwepo wa Mungu, kwa sababu wewe ni mdhambi kwa kuanzia.

Huwezi, haijalishi unafanya nini, uache kulewa, uache kuvuta, uache kusema uongo, nenda Kanisani na ujaribu kufanya hivi na ujaribu kufanya hivi, bado wewe ni watabia ya dunia. Hizo ni sheria tu, sheria haifanyi kitu chochote kikamilike. Lakini ni nini kinafanya ukamilifu? Ni Kristo. Utukufu. Ninaweza kuacha kusema uongo, niache kuiba, niache kufanya uzinzi, niache kutafuna, niache mambo yangu yote na bado mimi ni wa kimwili/kidunia. Mungu halipokei hilo, kwa sababu sina chochote cha kumtolea yeye ili kufanya upatanisho.

Lakini dakika ile ambayo ninaweka mikono yangu juu ya kichwa cha Bwana Yesu aliyebarikiwa na kusema Bwana, mimi sina uzuri wowote, je utanikubali kama mtumwa wako? Na Mungu anazisukumia mbali dhambi zangu, ninasimama mkamilifu mbele za Mungu. Hiyo ni kweli kwa nini? Sisimami kwa kustahili kwangu mwenyewe, ninasimama kwa kustahili kwake, na yeye ametukamilisha sisi kupitia mateso yake na Damu yake (Waebrania 10:14).

"Maana kwa toleo moja amewakamilisha (mpaka uamsho mwingine? Ningesemaje?) amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa". (waebrania 6:1-2) Unalipata hilo? Na tuendelee tuufikie utimilifu/ukamilifu.

Sasa, ninyi watu wa holiness mnasema – "Oh ndiyo tunaamini katika utakatifu. Haleluya , tunaamini juu ya utakaso". Lakini unachukuwa kwako mwenyewe. Unajaribu kuacha kile na kuacha kile, unajua hupaswi kufanya hivyo. Mpaka Kristo awe amekufungulia mlango, na kulihusisha hilo moyoni mwako, na unakuja

kuwa mahali ambapo dhambi imekufa, na shauku, zote zimeondoka (Waebr. 10:1-2) Hapo sasa anaondolea mbali haki ya kwako binafsi (Rumi 10:1-4) Naye anajijenga mwenyewe ndani yako. (Wakolosai 2:6-7) Na inakuwa ni Kristo, mwana wa Mungu ndani yako, tumaini la utukufu (Wakolosai. 1:26-27)

Hujaokolewa/kubadilishwa mpaka umepokea Roho Mtakatifu (Luka 22:31-32). Hiyo ni kweli. Unaamini ili kupokea ……… Roho Mtakatifu amezungumza na wewe, na umemkiri yeye hadharani. Shetani naye analo jambo hilo hilo. "Namwamini yeye kuwa ni mwana wa Mungu". Shetani hufanya hivyo. Lakini unatembea kumuelekea yeye. Wakati Petro alipoitwa na akahesabiwa haki kwa. Kumuamini Bwana yesu kristo ……. Na katika Yohana 17:17, Yesu aliwatakasa wao kupitia Neno, kwa maana Neno lilikuwa ni kweli, na yeye alikuwa ni Neno. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, Naye akakaa kwetu (Yohana Mt. 1:1-3, 14)

Yeye alikuwa Neno, hivyo aliwatakasa wao. Alisema, "Baba akizungumza na Roho iliyokuwa ndani yake), uwatakase kwa njia ya Neno". Yeye mwenyewe, akiwawekea mikono juu yao. "Neno lako ni kweli". Alinena neno, yeye akaumbika tumboni mwa mwanamke. Oh ni vigumu kabisa yeye awe kitu kingine zaidi ya hili Neno la Mungu, kumfanya yeye adhihirike. "Nina watakasa hawa".
Sasa, kuna mambo matatu pia katika ukamilifu wa hatua za neema kwa Kanisa. Kuhesabiwa haki kwa imani, kutakaswa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hayo pamoja hufanya kule kuzaliwa upya. Kama vile tu kuzaliwa kwa mwili kunavyo fanana na hiyo. Ambayo mwanamke anapomzaa mtoto, kitu cha kwanza kinachotoka ni maji, damu halafu uhai. Biblia ilisema katika 1 Yohana 5:7-8, Naamini ndiyo hapo ……. Ambapo panasema, "kuna watatu washuhudiao mbinguni, Baba, Neno (ambalo lilikuwa mwana) na Roho Mtakatifu. Watatu hawa ni mmoja. Kuna watatu washuhudiao duniani, Neno – maji, damu na Roho – maji, damu na Roho, hawa watatu hukubaliana katika jambo moja".

Sasa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni mmoja. Huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho mtakatifu. Lakini unaweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa. Unaweza kutakaswa bila kujazwa na Roho Mtakatifu, au unaweza kuwa na maji bila kuwa na Damu, na Damu bila Roho. Tumelithibitisha hilo – katika utaratibu wa maumbile.

Na kadhalika katika mambo ya kiroho. Ni maji, kuhesabiwa haki kwa Imani, kumuamini Mungu, kumpokea yeye kama mwokozi wako binafsi, na kwa kuwa umebatizwa (Yohana 1:12-13, Matendo 2:37-41), ya pili ni utakaso wa Roho, kwamba Mungu anaisafisha roho kutoka vitu vyote vya dunia na shauku za dunia na shauku za dunia, na baadaye Roho Mtakatifu anakuja ndani na kukupa kule kuzaliwa kwa pili na kukijaza kile chombo kilichotakaswa.

Kwa maneno mengine, mtu anakuja akipitia kule kuhesabiwa haki, anaendelea na kusema "ninaamini nataka kuhubiri Neno". Anaenda anaokolewa, anasema, "nimechoshwa na dhambi" hilo ni sawa. Halafu anaendeleo nje, na jambo la kwanza yeye bado anavuta, na pengine ana tamaa au kitu chochote baada ya muda anasema "Mungu, haya mambo hayastahili kwa Mkristo, hasa mhuduma, kuwaangalia wanawake katika mtazamo usio sahihi, kuvuta sigara" au ninachukua kinywaji cha ushirika cha bia pamoja na watu, Lakini – na hata washirika wa kusanyiko langu, lakini inaonekana siyo sahihi nitakase mimi Bwana". Hapo sasa Bwana anamtakasa anachukua tamaa zote ndani yake anaziondoa, kila kitu. Sasa anakuwa chombo kilichotakaswa. Sasa Mungu analolileta kwake ni ubatizo wa Roho mtakatifu. Kufanya hivyo inabidi atoke kwenye lile kundi alilonalo (2 Kor. 6:14-18). Hapo ndipo anapoonyesha rangi zake, hapo sasa anarudi nyuma. Anafanya nini hapo anaporudi nyuma? Anaikanyaga Damu ya Yesu Kristo iliyo mtakasa yeye, na kuihesabu kuwa ni kitu ovyo, kisichoweza kumvusha pale. Sasa ni vigumu kwa yeye kuokolewa. Sasa inamfanyia nini? Lakini kwenye kutazamia moto mkali na hukumu (Waebr. 10:26-29)

Angalia hili lilivyo zuri hapa. Tulikuwa tunalizungumzia hilo siku ile, angalia hapa, "Kwa hiyo tukiisha kuhesabiwa haki, kuhesabiwa haki itokayo katika imani (Rumi 5:1-2). Vyema sasa, sehemu ya pili, baada ya kuoshwa (Waefeso 5:25-27) kutakaswa na kujazwa na Roho Mtakatifu. Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaliona hilo? Ujumbe wake ulikuwaje? Kuhesabiwa haki kwa kusikia, utakaso ni kile wewe ufanyacho, na ni shukurani yako ya kuheshimu kile, Mungu alicho kitia Muhuri kwa Roho Mtakatifu (Waef. 1:13-14).

Hivyo ndiyo njia anayokuchukua wewe, kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa na kufa kabisa kupokea uzima (Amen). Siyo kwa dhehebu au kwa kanuni fulani, Lakini kupitia kifo cha roho yako, ili uweze kuzaliwa mara ya pili (Yohana 12:24-25)

Hii hapa inatufundisha sisi, kwamba Mungu anaweza kutumia kila sehemu ya mwili wetu kama imesalimishwa kwake. Anaweza akatumia akili zetu, ndoto zetu, sehemu yetu ya ubongo usiyodhahiri, ubongo wetu ndimi zetu, nyimbo zetu, macho yetu. Vyetu……….. Kila kitu tulicho nacho chaweza kutumiwa na Mungu kama kimesalimishwa kwa Mungu. Unaona? Kila kitu ulicho kisalimisha kwa Mungu. Atatumia kila kiwezekanacho na kila sehemu ya kwako, ataitumia. Haijalishi ni nini, ataitumia kama imetakaswa kwa kusudi lake na mwito wake.

Ulikuwa umebatizwa kwa ajili ya toba au kwa ondoleo la dhambi zako. Umekiri dhambi zako mbele za Mungu, na yeye amekusamehe hizo. Na wewe ukabatizwa kuonyesha kwamba umesamehewa, ukikiri mbele za watu na kuionyesha dunia kwamba unaamini kwamba Yesu kristo alikufa kwa ajili yako, na akachukua mahali pako, na sasa unasimama mahali pake. Amekuwa wewe ili wewe uweze kuwa yeye. Ndipo nguvu za utakaso za Mungu zinakusafisha tabia zote za maisha yako. Ulizoea kuvuta, kulewa, kufanya mambo yasiyosahihi, kusema uongo, na kila kitu. Ndipo ile nguvu ya utakaso ya Damu ya Yesu Kristo inakuja katika maisha yako. Inaondoa vitu vyote mbali na wewe (Warumi 15:16). Kama ukitokea kusema, kuna kitu hakiko sahihi, haraka unasema "subiri kidogo,

nisamehe mimi, sikumaanisha kusema kama hivyo" Unaona? Shetani amekuwekea mtego pale, lakini unayo neema ya kukufanya urudi nyuma kama wewe ni Mkristo halisi na kusema "nilikuwa nimekosea". Ndiyo kwa hiyo…………………… .

Sasa kitu kinachofuatia unapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na moto (1Kor. 12:13, Matayo 3:11-12).

Huu ni ujumbe wangu kwa Kanisa sasa. Ninyi mmesimama, kama umesimama katika neno la Mungu na unalo Neno la Mungu, kila amin, kila nukta, kila kitu kadogo. Umesimamia wapi? Ninajaribu kukueleza wewe, toka katika hayo makapi na uingie hapa katika ngano ambapo utakomazwa kwa kukaa juani. Nasikia ile mashine ya kuvunia inakuja. Umesimama ukiwa umekamilika, ukiwa umehesabiwa haki kama hujafanya lolote kwa kuanzia. Haleluya. Zungumza kuhusu kutoa shukurani. Najisikia vizuri sana, nashukuru kwa hilo zaidi ya kitu kingine chochote nijuacho. Ninyi ni Bibi arusi wa mwana wa Mungu aliye hai, safi na Bikira, asiye na dhambi yeyote. Kila mwanamume na mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, na akaoshwa katika Damu ya Yesu Kristo, na kuamini kila Neno la Mungu, unasimama kama vile hujawahi kutenda dhambi hata kidogo tangu mwanzo wewe ni mkamilifu. Ile Damu ya Yesu Kristo ………………….. .

Mtu anapompokea Kristo kama mwokozi wake, kila kitu (kinafurahi) kama yuko juu ya nyumba. Kila kitu ndege wanaimba tofauti, na kila kitu ni kizuri. Na jamani mimi jinsi kila kitu kilivyokuwa kizuri mara ile ya kwanza ulipookolewa. Ukaja ule wakati wa majaribu, wakati wa kuadabishwa, wakati wa kutakaswa, kujitakasa mwenyewe kutoka kwenye mambo ya dunia, "kuweka kando kila mzigo na dhambi ile ituzingayo kwa upesi" (Waebrania 12:1-2). Wewe mwanaume ilibidi uache kuvuta sigara, uache ulevi, uache kwenda kwenye vyumba vya kuogelea, karamu zako za usiku kucha, mambo haya yote, ilibidi ujitakase mwenyewe kutoka mambo hayo kwa imani katika Damu ya Yesu Kristo (Matendo 26:18) kujitakasa mwenyewe. Ninyi wanawake ilibidi muache nywele zenu zikuwe upya, nguo zenu mlizirefusha, na mtende tofauti na mlivyokuwa, wakati wa kutakaswa. Mara nyingi wangeasi na kurudi nyuma, vyema huyo siyo mtoto wa Mungu. Unaona? Mtoto wa Mungu anaangalia moja kwa moja msalabani naye anajua yote ni katika kumpatia mema..
Lakini kabla mtu huyu hajaja kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, mtu huyu, lazima apitie wakati wa utakaso. Lazima afikie wakati wa kujaribiwa katika maisha yake. Kila mmoja amepitia hilo. Amekuwa na wakati wake wa kujaribiwa. "Kila mwana ajaye kwa Mungu, ni lazima kwanza arudiwe, aonywe, afunzwe na kama hatuwezi kustahimili kurudiwa, hiyo ni dhahiri kuwa sisi siyo watoto wa Mungu, tu wana wa haramu na siyo wana wa Mungu" Biblia ilisema (Waebrania 12:4-11). Lakini kama tunaweza kustahimili marudio kwa kujua kwamba mambo yote yanatenda kazi katika kuwapatia mema wale wampendao Bwana (Warumi 8:28) hapo sasa, tu wana na binti za Mungu. Sasa anatutia muhuri na Roho Mtakatifu mpaka siku ya ukombozi (Waefeso 4:30) unaona. Huko ndiko kurudiwa, jambo la kuumiza, mambo tunayoyapitia.

Kwa hiyo, hakuna Damu nyingine itakasayo watu (Waebr. 13:12) siwezi kukutakasa wewe, nawewe huwezi kunitakasa mimi kwa sababu wote tumezaliwa kwa namna ya kujuana kimwili. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo Damu yake ni chombo cha kutakasia. Na Mungu akashuka chini, akafanya mwili, akaishi ndani yake, akamwaga hiyo damu kwa kutakasia, na kwa hakika inaiondoa dhambi mbali na aibu (Waebr. 10:5-14)

Sasa hatua ya kwanza ni toba kumuelekea Mungu, na kinachofuata, ni ubatizo wa maji. Ubatizo wa maji "Tubuni mkabatizwe kila mmoja katika jina la Yesu Kristo" (Matendo 2:37-41) Unaona? Ubatizo wa maji unafuatia ukionyesha kuwa hiyo toba ilikuwa ya kweli au, kuondoa dhambi zetu zilizopita. Sasa hilo halina uhusiano na dhambi za baadaye (Wagalatia 6:1, 1Yohana 1:8-10, 1Yohana 2:1-2). Inaondoa tu. "Tubuni na mbatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo". Kwa nini? Kwa ondoleo, kuziondoa dhambi za nyuma. Hilo halihusiani na mambo ya mbele. Dhambi zako za nyuma zimeondolewa, yale uliyotenda.

Huwezi ukatubu kwa dhambi alizozifanya Adamu. Hukufanya wewe, Adamu ndiye alifanya. Unapata msamaha kwa lile ulilolifanya. Lakini ile asili ya zamani iko pale. Hebu nichukue ubao huu kwa dakika chache.

Sasa hapa ni moyo wa binadamu. Mimi niko mbali sana katika uchoraji. Unaona? Hapa ni moyo wa mtu, na hapa ni moyo wa mtu. Sasa huu mmoja hapa una nyoka ndani yake, hiyo ni dhambi. Huyu hapa ana uzima. Huu mmoja hapa unahua ndani yake, ambaye ni Roho Mtakatifu (Matayo 3:16-17). Hapa ana uzima, vyema huyu mmoja hapa ana uovu, chuki, wivu. Hiki ndicho kinacho sababisha huyu kiumbe hapa. Vyema huyu mmoja hapa anaupendo na furaha, na mvumilivu na huyu ndiye anayesababisha hayo hapa.

Sasa unapoulizwa wakati……au wakati unaposamehewa dhambi zako, umefanya tu hili, lile limeondolewa mbali. Lakini kitu kile kilichokufanya ufanye jambo hilo bado kipo pale. Huo ni huo mzizi wa zamani wa uovu. Bado uko pale.
Angalia sasa hatua ya pili unakuja utakaso, ambao unaweka akili au Nia yetu katika utaratibu wa utakatifu: Kufikiri kwa usahihi, kuondolea mbali. Utakaso ni Neno la kigiriki lenye maana mbili, ambayo ni "iliyosafishwa na kuwekwa kando kwa huduma". (Mithali 23:7, Zaburi 51:10-12).

Sasa angalia Utakaso, hatua yake ya pili, inasafisha nia na kuuweka moyo, ile nia ya moyo inakuwa kwenye utaratibu wa utakatifu.

Mtu anaweza akatubu dhambi na bado anaifikiria ……………. Vyema, pengine ni mtu mwenye tabia mbaya kila mwanamke mzinzi anayeonekana kumwangalia, hilo liko pale. Pengine ni mlevi, kila mara anaposikia harufu ya pombe, bado iko pale. Unaona? Lakini sasa anapotakaswa, hiyo inaondoa hiyo shauku kutoka

ndani yake. Unaona? Inaondoa mbali ile tamaa (Waebr. 10:1-2). Anaweza bado akajaribiwa, lakini anaondolea mbali ule uhitaji wa hilo. Na hata yeye hayuko sahihi bado. Baadaye anabatizwa na Roho Mtakatifu na moto (Matayo 3:11). Ameoshwa, na kuchomwa, amesafishika na kuwekwa kwenye huduma ya Mungu. Utakaso unamtayarisha na kumuweka tu tayari kwa huduma.

Ubatizo wa Moto na Roho Mtakatifu kwamba Mungu aweze kukaa ndani yetu na moto wa Mungu unasafisha mioyo yetu kutoka kwenye dhambi na kumuweka Roho Mtakatifu ndani (Matendo 2:1-4; Matendo 4:31) Halafu tunakuwa na maisha yale yale ambayo Huyo alifanya kwa sababu huyo yuko ndani yetu.

Fikiria, mavazi yako yameoshwa kwa maji ya Neno linalomwagika damu (Waefeso 5:25-27) Lile Neno limekuwa Damu. Neno litoalo Damu (Yohana 1:1-3,14). Lile Neno likitoa Damu, maisha ya Mungu ndani ya Neno, na Neno lilitoa Damu kwa ajili yako. Ili kwamba uoshwe kutoka kwenye uchafu wa hawa makahaba na usafishwe na kutakaswa kwa kuoshwa kwa maji ya Neno ambalo linaifanya nia yako na moyo wako vikae ndani ya Mungu na juu ya Neno lake.

Nabii wa Mungu katika maombi:
Bwana, katika Nuru ya Neno Lako, namuamuru kila mtu ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo aharakishe upesi majini wakati kuna nafasi. Ninyi ambao hamjajazwa na Roho Mtakatifu, nawaamuru katika Jina la Bwana Yesu Kristo angukeni kwenye magoti na msiinuke juu mpaka Roho Mtakatifu amewatakasa ninyi vizuri kabisa na kuwajaza ninyi na Roho Wake na uzuri wake mpaka nafsi yako imetoshelezwa katika uwepo wa Mungu na kuwa shauku yako yote ni kumtumikia Yeye na kuishi kwa ajili Yake na kutenda kazi pamoja naye muda wote uliobakia wa maisha yako. Tujalie hilo, naomba kwamba Mungu atawawajibisha hilo, katika Jina la Yesu Kristo.

2Kor.7:1: Basi wapenzi wangu kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.

Baba yetu wa mbinguni, tunainamia uweponi pako kwa niaba ya hawa walioko madhabahuni. Acha neema yako iwe juu ya kila mmoja wao, Baba. Sasa, kama, Bwana ………. Siwezi kulifanya hilo kwa ajili yao. Inawapasa walifanye hilo wao wenyewe. Hakuna awezaye kulifanya kwa ajili yao. Inabidi walifanye peke yao. Wacha nafsi zao waliseme wao wenyewe oh Mungu, hii hasira naiweka hapa chini Bwana; sitaichukua tena. Haijalishi kuna kuja nini au kunakwenda nini, ninaiachia iende kutoka sasa na kuendelea. Huu ulimi wangu umekuwa mwepesi kuchukua upande na kundi la wasengenyaji Bwana. Hebu ruhusu niwasikie malaika wakiingia ndani kama vile Isaya alivyofanya hapo aliposema, “mimi ni mtu mwenye midomo michafu ole wangu”. Na malaika wakaja, wakachukua makoleo na kwenda madhabahuni, na kuchukua makaa ya moto, na kuliweka mdomoni mwake na kuitakasa”. Mungu, takasa kila anayezungumza asubuhi hii na leo ambaye anazungumza mambo yasiyosahihi na kupanda kutoelewana. Jalia hilo Bwana.

Kuona moto wa uamsho unaanza kufifia, na tutupe kuni za Neno, ambazo zitawasha tena moto mpya, kwamba mioyo yetu itajaa juhudi, tutakase sisi, Bwana, kupitia Neno lako la thamani, na Damu yako, na Neema yako tunasihi; na shukrani na sifa zote zitakuwa zako. Ondoa udhalimu wote kutoka mioyo yetu; tusafishe sisi oh Bwana. Tupe mioyo myeupe, na uoshe mikono yetu, na nia zilizo safi; kwamba tuweze kuja mahali pako patakatifu usiku baada ya usiku, tukifurahi na kujazwa na Roho Wako. Tunaomba hili katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

Nukuu za Kiingereza
Ukamilifu para 77-83, 30; Waebrania sura 7 sehemu ya 2 para 366
Waebrania sura ya 5 na ya 6 para 128, Roho Mtakatifu ametolewa kwa nini?
Para 54, 85, ile mbegu haitarithi pamoja na kapi Para 49-50
Maswali na majibu (61-1015 m) {para 79; ufunuo sura ya 4 sehemu ya 3
(Kiti cha rehema) Aya 211, vipawa vya Mungu hutafuta mahali pake Aya 41
Mambo yatakayokuwa aya 63-64; kuachilia Presha Aya 124.
Muungano wa siri uk. 37, 38, maji yakudumu yatokayo mwambani Aya 67-68
Makao ya baadaye uk. 15-17; uchungu wa uzazi uk.8
Muhuri wa pili kitabu cha mihuri uk. 226
Roho zidanganyazo Aya 147; Roho Mtakatifu ni nini? Aya 17.

---

Jiwe la kujenga la kiroho no. 128. Kutoka Neno la saa hii iliyokusanywa na Gerd Rode wald, Friedenstr.69 D75328 Schomberg, Germany Phone (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya harka itaizunguka dunia. Zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo. Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*